



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA  
WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA  
LESENI



**UWASILISHAJI WA TAARIFA ZA WAMILIKI MANUFAA WA MAKAMPUNI**

**Dar es Salaam- 11 Mei, 2022**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) inawakumbusha wamiliki wa makampuni yaliyosajiliwa hapa chini kuwa tarehe 30 Juni, 2022 ni siku ya mwisho ya kuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa. Taarifa hizo zinatakiwa kuwasilishwa kupitia tovuti ya BRELA ([bo.brela.go.tz](http://bo.brela.go.tz))

Serikali kupitia Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara mnamo mwezi Januari mwaka 2022, iliongeza muda wa miezi sita (6), ya uwasilishaji wa taarifa hizi ili kuwawezesha wamiliki wa makampuni kuteleza kwa ukamilifu takwa hilo la kisheria.

Uwasilishaji wa taarifa za Mmiliki Manufaa una lengo la kuboresha mazingira ya uwekezaji, kuzuia rushwa na utakatishaji fedha, kuongeza utekelezaji wa sheria, kujenga uaminifu na uwajibikaji na hatimaye kuongeza pato la Taifa.

Kwa taarifa hii BRELA inawataka wamiliki wa makampuni ambao bado hawajawasilisha taarifa zao kufanya hivyo katika siku zilizosalia ili kuepuka usumbufu usio wa lazima.

Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana nasi kwa simu Na: +255 (0) 222 212 800 au barua pepe [usajili@brela.go.tz](mailto:usajili@brela.go.tz), mitandao ya kijamii: Instagram na Twitter [brela\\_tanzania](https://www.instagram.com/brela_tanzania), Face book: BRELA Tanzania au tembelea tovuti ya BRELA: [www.brela.go.tz](http://www.brela.go.tz)

**Imetolewa na;**

Kitengo cha Habari na Mawasiliano